



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA



Mkoa wa Singida.  
Simu Na. 0262502252/2237  
Fax Na. 0262502719  
Barua pepe: [ded.singidadc@singida.go.tz](mailto:ded.singidadc@singida.go.tz)

S.L.P. 27,  
SINGIDA.

Kumb.Na. SDC/B.1/50/ PART 'F' 129

Tarehe: 25/02/2025

### **TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA .**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Singida anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, katika (Vituo vya Afya ) , Kuomba nafasi ya kazi ya mkataba wa Mwaka mmoja kama ifuatavyo;

#### **1.0 KAZI YA MSAIDIZI WA HESABU DARAJA II NAFASI 02.**

##### **1.1 SIFA ZA MUOMBAJI.**

- Kuajiriwa wenye cheti cha Astashahada ya uhasibu kutoka chuo kinachotambulika na Serikali au cheti cha ATEC 1 kilichotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA.

##### **1.2 KAZI / MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA HESABU DARAJA LA II**

- Kuandika na kutunza kumbukumbu zinazohusu shughuli za uhasibu
- Kutunza kumbukumbu za hesabu
- Kupeleka barua / nyaraka za uhasibu Benki
- Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi

##### **1.3 MSHAHARA.**

- Ngazi ya Mshahara ni **TGS B**

## 2.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wanatakiwa wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia Miaka 18 hadi 45
- ii. Waombaji wote waambatanishe Cheti cha Kuzaliwa
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed CV**) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**Referees**) wawili.
- iv. Maombi yote yaambatane na picha **1 ( Passport Size )** , Nakala za Vyeti Taaluma Vyeti vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na Vyeti vya kuhitimu Mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoelekezwa hapo juu.
- v. Waombaji wote waambatanishe Nakala za Kitambulisho cha Taifa (**NIDA**) kwa ambao hawana Vitambulisho hivyo , Namba za NIDA ziandikwe kwenye maelezo binafsi (**CV** )
- vi. Testimonials "Provisional Results", "Statement of Results", hati matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) havitakubaliwa.
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (**TCU NA NECTA**).
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Mamlaka husika.
- ix. Maombi yaliyowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika Tangazo hili hayatafikiriwa.
- x. Maombi yote yatumwe kwenye Anuani ifuatayo ;

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P 27,  
SINGIDA.

**N.B: Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 10/03/2025.**

Imetolewa na



Janeth Mbuga  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
SINGIDA.**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
SINGIDA**

**Nakala:** Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya Singida  
[singidadc.go.tz](http://singidadc.go.tz)

**Mbao za Matangazo**